Najua Mkombozi Wangu Yu Hai

. . . siku zote takatifu, hii ndiyo siku, siku ya ufufuo. Kuja pamoja kwa furaha ya moyo, kwa sababu Yeye yu hai. Naye akasema, “Kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mnaishi.” Na hilo ni tumaini jinsi gani, ambalo tunaweza kutulia juu yake, asubuhi ya leo.

2 Sasa kabla tu hatujapata Ujumbe wa asubuhi, hebu na tuinamishe vichwa vyetu, mbele kidogo tu, kwa ajili ya maombi.

3 Mungu Mpendwa, tunashukuru asubuhi ya leo, kuwa ndio watu wanaoitwa kwa Jina Lako. Tuna furaha sana kwamba hatuhitaji kuwazia tu, tena, juu ya ufufuo mkuu utakaokuja; kwa sababu imekuwa kweli kwetu, tunapoisoma katika Neno Lako, na kuona ya kwamba Wewe umeahidi jambo hili, na kuhisi ndani ya nafsi zetu, kwamba Yesu anaishi- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

4 Loo, tunawazia, asubuhi ya leo, juu ya huzuni nyingi ambazo zimekuwa katika maisha, na masikitiko mengi ambayo tumepitia, na matukio ambayo yametuvuruga, na kututupa kwenye pepo za dunia. Jinsi tulivyowazika wapendwa wetu, na tumeomboleza kaburini. Nazo na—nafsi zetu zinaonekana kukaribia kuangamia ndani yetu. Lakini, basi, tunaweza kufikiria leo, loo, inamaanisha nini kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu! Aliharibu kila nguvu ya adui, alipofufuka, akashinda. Aliondolea mbali vivuli vyote. Sasa tunatembea katika nuru ya thamani ya ufufuo Wake.

5 Loo, tunaweza kuwazia, miaka elfu moja na mia tisa, ama zaidi, asubuhi ya leo, wakati maskini wanawake wawili wakiwa njiani kuelekea kaburini, wakishangaa ni nani angeliondoa jiwe. Lakini Mungu alikuwa tayari ameliondoa. Naye Yule aliyekuwa amezuiliwa, alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu na kusema nao. Na akasema, “Nendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu, na Petro, ya kwamba nitakutana nao huko Galilaya.”

6 Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya tukio hili kuu, kwamba bado tunaweza kushuhudia ufufuo huo, na inakuwa halisi tu kwetu kama ilivyokuwa kwao asubuhi ile, kwa maana amefufuka kutoka kwa wafu.

7 Utusamehe dhambi zetu na kupungukiwa kwetu, yote tuliyofanya au kusema, au hata kuwaza, ambayo yalikuwa mabaya, Bwana. Tunaomba ya kwamba utatusamehe kwa mambo haya. Na ututie muhuri, kwa kilindi. Sogea karibu,

asubuhi ya leo. Loo, mara nyingi Wewe unasimama katika vivuli, wakati shida zetu ni za kilindi sana.

8 Mariamu alipogeuka kutoka kaburini asubuhi ile, akawa analia, naye akasikia Sauti nyuma yake, ikasema, “Kwa nini unalia?” Alikuwa tu nyuma yake, akitazama tu kilichokuwa kinaendelea. Na wakati Yeye aliponena jina lake, jinsi moyo wake hapana shaka uliruka kwa furaha, kwa maana Bwana wake alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu.

9 Loo, sema nasi asubuhi ya leo, Bwana. Utupe Neno Lako na Roho Wako. Na utupe hakikisho, upya, asubuhi ya leo, tunapozungumza juu ya manabii na wale mbalimbali waliongojea wakati huu mkuu.

10 Nasi tunangojea ufufuo wa jumla katika siku za mwisho, wakati Bwana wetu atakapokuja tena. Hadi wakati huo, Bwana, utudumishe wenye afya, furaha, wenye furaha tele, tukishangilia. Wala si kuishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, na tufanye riziki yetu. Utujalie, Baba, kwa maana tunaomba katika Jina Lake, Yeye aliyefufuka kutoka kwa wafu na kutoa hakikisho la ufufuo wetu. Amina.

11 Nilipokuwa nikishuka barabarani muda mfupi tu uliopita, nami nilikuwa nikiwazia, ndege walipokuwa wakiimba, ni majira ya kuchipua jinsi gani leo! Baada ya. . .Jinsi Pasaka inavyofaa! Baada ya majira ya baridi kali yenye giza na baridi kupita, na vimbunga vyake vyote na kadhalika, ndipo mwanga wa jua unaanza. Na kuja kwa jua huleta maisha mapya, matumaini mapya, misimu mipya, mazao mapya, maua mapya. Kila kitu huja kwa uzima. Jinsi ambavyo mtu, hata ambaye hakuwa na Biblia ya kusoma, angeweza bado kujua kwamba kuna Mungu. Wakati aliweza kutazama tu maumbile, jinsi yanavyoenda na kuja; msimu wa kupukutisha wa mwaka ni kusulubiwa; msimu wa kuchipusha wa mwaka ni ufufuo; na inamwona Mungu tu katika kila kitu.

12 Nami nilikuwa nikiwazia, nilipokuwa nikisikia ndege wangu wadogo wakiimba, nje uani asubuhi ya leo, robini wangu wadogo, kwa vile mimi ninawapenda tu. Ninawaita redio zangu ndogo. Nami natoka na kuwasha redio yangu, asubuhi, kuisikiliza.

13 Na, sasa, unajua hadithi ndogo ya robini. Alikuwa ndege mdogo wa kahawia, kulingana na hadithi, hadi Ijumaa Kuu. Na kulikuwa na Mmoja anayekufa, peke yake, na hapakuwa na mtu wa kumsaidia. Naye akasimama peke yake. Naye alipigiliwa misumari, na msalabani. Na ndege mdogo wa kahawia alikuwa akijaribu kumweka huru kutoka msalabani. Na katika kupiga mbizi huku na huko, kwenye misumari, na kwa miiba juu ya kichwa Chake, alifanya maskini kifua chake kuwa chekundu kabisa kwa damu, na tangu wakati huo kimekuwa chekundu.

Na nilifikiria, “Ee Mungu, hiyo ndiyo aina ya ngao ninayotaka.”

14 Na ikiwa utaona robini mdogo wakati anajidonoa mwenyewe. Chini tu ya hiyo rusu ndogo nyekundu ya manyoya, kuna weusi, ni manyoya yake mengine. Lakini—ngao nyekundu inamlinda.

15 Hiyo ndiyo ninayotaka. Haijalishi jinsi tungejaribu kuwa wema, tungali ni wenye dhambi. Lakini ngao hiyo ndogo tu nyekundu ndiyo inahitajika kumfanya awe tofauti na ndege wengine. Hilo ndilo tu linalohitajika kutufanya tuwe tofauti na ulimwengu, ni hiyo ngao ndogo tu, nyekundu ya neema Yake.

16 Tunakuja asubuhi ya leo kwenye Pasaka, kama kila asubuhi ya Pasaka tunayotazamia, kukusanyika katika mapambazuko haya ya jua. Na imekuwa ni majaliwa yangu, kwa miaka mingi iliyopita, kuja hapa maskanini na kuwabatiza watu, na kuwahubiria kufufuka kwake Bwana Yesu.

17 Na nilipokuwa nikisoma, jana jioni, wakati wa dhoruba, na nilikuwa nikiwaza, “Je, ni maneno gani yangefaa kusemwa, asubuhi, kwenye ibada hii ya ufufuo?” Na mawazo yangu yakaangukia somo hili ambalo ndugu yetu amesoma hivi punde, la Ayubu mlango wa 19, na ki—kifungu cha 23 hadi cha 27. *“Najua Mkombozi Wangu Yu Hai,”* alisema Ayubu. Na nilichagua hilo kwa ajili ya somo.

18 Na tunapokuja, kwa nini tunakuja? Ni kwa kusudi hili, pekee, kwamba tunaweza kupata matumaini mapya.

19 Tuko katika dunia hii hapa, na tunajua tunaishi gizani. Hatupaswi kufikiria kwa namna fulani mambo haya, au kujidanganya wenyewe, kama ilivyokuwa, kwa sababu tunajua kwamba tunaishi katika vivuli vya mauti. Kila wakati tunaposikia kilio cha gari la kuchukulia wagonjwa, tunapopita makaburini, tunapoona hospitali, kila mvi, inatia alama kwenye kumbukumbu zetu kwamba sisi ni watu waliohukumiwa, kwa wote vijana kwa wazee.

20 Nasi tunakuja asubuhi kama hii, kukusanya matumaini, matumaini mapya ya kile kilichotuleta hapa, na kilicho kusudi. Na ninafikiri kwamba huu ni wakati mzuri sana wa kufikiri juu ya matumaini ambayo Mungu ametupa. Sasa tunataka kuchora hii, kwanza, katika akili zetu, kwamba hakuna kitu chochote kinachoweza kutuangamiza mpaka kusudi la Yeye aliyetuumba litimie. Huenda kusiwe na chochote. Tumeumbwa kwa kusudi.

21 Kanisa hili lilijengwa hapa kwa kusudi fulani. Msingi huu haukuchimbwa, na jiwe la msingi kuwekwa, na matofali kuwekwa kwenye je—jengo, na paa na vitu vya ndani, havikuwekwa hapa ili tu kuona ikiwa inaweza kufanywa. Iliwekwa hapa kwa kusudi, ama kwa kusudi fulani.

22 Nyumba yako unayoishi, haikuwekwa hapo kwa bahati mbaya tu, au mtu fulani kupoteza muda tu. Nyumba yako ilijengwa kwa kusudi, kutimiza kusudi fulani.

23 Kama uliendesha gari, asubuhi ya leo, kuja hapa, kwenye gari lako, gari hilo halikutengenezwa ili tu kuona kama lingeweza kutengenezwa. Nyenzo hazikuharibiwa na mwanadamu. Iliwekwa hapa kwa kusudi, na kutumikia kusudi fulani.

24 Mavazi unayovaa, haikuwa tu kuona kama mtu anaweza kutengeneza kitu. Ilikuwa kwa kusudi fulani.

25 Chakula unachokula, hakikukuzwa ardhini ili kuona tu kinakua. Kilifanywa ili kutimiza kusudi fulani.

26 Na Mungu hakuhitaji kuumba mti tu ili uwe mti. Aliumba mti kwa kusudi fulani.

27 Na Mungu hakutuumba mimi na wewe, ili tu kuona kama angeweza kufanya jambo hilo. Alituumba kwa kusudi fulani. Kwa hiyo, kuna kusudi la sisi sote kuwa hapa. Huko hapa ili tu kuwa mwanadamu mwingine. Upo hapa kwa sababu Mungu alikuumba kwa kusudi fulani. Huko hapa kula tu chakula ambacho Mungu alikuza. Huko hapa ili kuishi tu katika nyumba ambayo—ambayo mtu alijenga, au kuvaa mavazi ambayo mtu fulani alitengeneza. Uko hapa kwa kusudi maalum. Haijalishi wewe ni mdogo kiasi gani, wewe ni mkubwa kiasi gani, wewe ni muhimu kiasi gani, au jinsi ulivyo duni, uko hapa kutumikia kusudi fulani.

28 Kama vile, kidole changu kiko hapa kwa kusudi fulani. Ukucha wangu kwenye kidole changu ni kwa kusudi fulani. Jicho langu, na kila sehemu ya miili yetu, ni za kutumikia kusudi fulani. Na haikuwekwa hapa ili tu kuona jinsi itakavyokuwa wakati iliwekwa hapa, lakini iliwekwa hapa ili kutimiza kusudi lake. Ulikuwa ni mpango wa Kiungu wa Mungu kufanya hivyo.

29 Na ikiwa tuliwekwa hapa kwa kusudi fulani, basi hakuna kitu kinachoweza kutuangamiza hadi kusudi la Mungu litimie. Hakuna kitu kinachoweza kutudhuru mpaka kusudi hilo, ambalo Mungu ametuwekea hapa, limedhihirishwa. Haijalishi tuna shida kiasi gani, ni huzuni nyingi kiasi gani au huzuni tunayopitia, hizi zote ni sababu, na kuna sababu yake.

30 Tutachukua, kwa mfano, Nuhu, katika Biblia. Kulikuwa na gharika iliyokuja, na dunia yote ikaharibiwa. Mimea na kila kitu viliharibiwa isipokuwa Nuhu na uzao ambao alikuwa ameingiza ndani ya safina.

31 Kusudi la Mungu haliwezi kushindwa kamwe. Hakuna kinachoweza kulishinda. Kwa hiyo tunapaswa kuwa na furaha jinsi gani leo, tukitulia juu ya ule ufunuo mzuri wa Neno la Mungu aliye hai, kwamba hakuna mambo yaliyopo, wala yanayoweza kuja. Hakuna magonjwa, hakuna huzuni, hakuna

kifo, hakuna hatari, wala hakuna chochote kinachoweza kututenganisha na kusudi la Mungu aliye hai. Yale ambayo Mungu ameyawazia katika nia yake, yale ambayo Mungu amekusudia moyoni mwake, kutimiza; hakuna pepo, hakuna nguvu, hakuna kitu kinachoweza kutenganisha mpango mkuu wa Mungu usioweza kufa, wa Milele. Ni lazima iwe kama Mungu alivyosema.

32 Ndipo tunaona, ya kwamba katika siku ambazo ulimwengu wote ungeangamizwa kwa gharika, kwamba Mungu alifanya maandalizi. Maandalizi kwa sababu gani? Ili kuhifadhi kusudi Lake. Alifanya hivyo katika siku za Nuhu.

33 Naye anafanya hivyo leo. Amefanya maandalizi, kuhifadhi kwa kusudi Lake mwenyewe. Atahifadhi Kanisa. Atawahifadhi watu. Atahifadhi raia kwa ajili ya milki Yake kuu, ambayo kifo hakiwezi kuangamiza. Na tunatambua ya kwamba ni kwa imani tunaamini hili, lakini ufufuo huleta msingi imara ambao imani yetu inatulia juu yake. Hakuna kinachoweza kuiharibu. Kama mshairi alivyoandika wakati mmoja:

> Loo, ni kionjo jinsi gani cha utukufu wa Kiungu!
> Mrithi wa wokovu, aliyenunuliwa na Mungu,
> Nimezawa kwa Roho Wake, nikaoshwa kwa Damu Yake.

34 Ni hakikisho la jinsi gani, juu ya Mwamba huu imara, ufufuo wa Mpenzi wetu aliyebarikiwa, Bwana Yesu. Hakuna kinachoweza kuiharibu. Imepandwa. Ni Uzao wa Mungu. Ni kusudi la Mungu kutupa Roho Mtakatifu aliyebarikiwa. Ni kusudi la Mungu kutuonyesha ishara na maajabu na miujiza. Ni kusudi la Mungu, na hakuna kinachoweza kuliharibu. Nguvu zote za kuzimu zinaweza kupigana nayo, lakini itashinda. Tuna ahadi ya Milele ya Mungu. Kunaweza kuwa na walimu, kunaweza kuwa na itikadi kuinuka, kunaweza kuwa na mipango mikubwa kuinuka, kunaweza kuwa na mambo ambayo yanaonekana kama kwamba ingeharibiwa, lakini haiwezi kuharibiwa kamwe. Ni kusudi la Mungu kuona kwamba itashinda. Kisha, sio juu yangu, na sio juu yako, ikiwa itaharibiwa au la. Ni juu ya Mungu. Nasi tunaweza kuwa na uhakika juu yake, ya kwamba Mungu hataacha urithi wetu uharibiwe, kwa maana ni kusudi Lake kutupa sisi.

35 Sasa tungefikiria, pia, leo, juu ya maangamizi, kujaribu kuangamiza. Tunayo ahadi ya Kristo mwenyewe.

36 Tunawakumbuka watoto wa Kiebrania, wakati Mungu alikuwa na kusudi kwa ajili yao. Walipokuwa huko Babeli, na ile tanuru ikawashwa moto mara saba kuliko ilivyopata kuwashwa, kuharibu kusudi la Mungu. Na Babeli yote ilikuwa na ghadhabu. Walikuwa wamedhamiria, Shetani alikuwa, kuharibu kusudi la Mungu, kwa maana alijua watoto hao walikuwa wakiingia

kwenye tanuru. Kwa hiyo akaifanya tanuru, walipoitia moto, kuwa moto zaidi mara saba, ili kuhakikisha kwamba mpango wa Mungu ungeharibiwa. Lakini Mungu alitaka kuonyesha uwezo Wake, na Babeli yote na kuzimu yote havingeweza kulishinda kusudi hilo. Hapana, bwana. Haijalishi kama wangeweza kuipasha tanuru hiyo moto zaidi mara milioni, haingeharibu kusudi la Mungu kamwe. Mungu alitaka kuonyesha kwamba Yeye alikuwa ni Mungu wa ukombozi, Naye angeleta ukombozi kwa yeyote aliyetaka kuuleta, na hakuna kitu kingeingilia mpango Wake.

37 Basi walipoitia moto tanuru, Shadraka, Meshaki na Abednego hawakujua kwamba walikuwa wanatoka kwenye tanuru ile. Kwa maana walisema, wenyewe, "Mungu wetu anaweza kutukomboa. Lakini, hata hivyo, hatutaisujudia sanamu hiyo." Mungu alikuwa na mtu ambaye angemtumikia, na kusudi Lake halingeshindwa. Moto hauwezi—hauwezi kulishinda kusudi la mpango wa Mungu.

38 Na, loo, jinsi ninavyopenda kusema jambo hili, asubuhi ya leo. Mabomu yote ya haidrojeni duniani hayawezi kamwe kushinda ufufuo wa Kanisa Lake. Kueleza vinginevyo kwote, na hisabati yote, na—na kadhalika, ambayo ulimwengu huu wenye akili umeleta kwa ujanja, kupitia kusudi lake la kufanya jambo fulani, kuharibu imani ya watoto wa Mungu, haitafanya hivyo kamwe. Imani hiyo itadumu milele.

39 Ilikuwa ni kusudi la Mungu kuonyesha kwamba alikuwa na mamlaka juu ya hayawani-mwitu wa porini. Na wakaweka simba katika pango wakati mmoja. Na walikuwa wamewanyima chakula mpaka wakawa na njaa sana, hata wangeweza kurarua m—mtu vipande vipande, kwa nyakuo moja kubwa tu. Na shetani akawaza, "Hakika, nitaweza kumwangamiza nabii huyu, Danieli."

40 Lakini Danieli alikuwa amekusudia moyoni mwake kufanya kusudi la Mungu. Na Mungu alikuwa ameweka hilo moyoni mwake. Kabla Danieli hajaweza kuwa na shauku hiyo, ilibidi kuwe na kitu cha kuunda shauku hiyo. Kabla ya kuwa na imani hiyo, ilibidi kuwe na kitu cha kumwambia kwamba kulikuwa na Mungu ambaye angeweza kukomboa.

41 Na, loo, jinsi hilo linavyoingiana asubuhi ya leo, na imani, imani iliyo hai ya Mungu aliye hai, katika Kanisa Lake. Kuna kitu ndani ya mioyo yetu kinachosema kwamba kuna Nchi ng'ambo ya mto. Siwezi kuweka kidole changu kwenye Nchi hiyo, na wala mwanadamu yeyote hawezi, lakini kuna kitu ndani yetu ambacho kinatuambia kwamba:

> Kaburi si lengo lake;
> Na wewe u mavumbi, utarudi mavumbini,
> Haikunenwa juu ya nafsi.

42 Kuna kitu ndani yetu, moto unaowaka, nuru ambayo imewashwa na Mungu, na hakuna upepo unaoweza kuizima. Hakuna nyakati za baridi kanisani, hakuna kutokujali miongoni mwa watu, hakuna mateso ya ulimwengu, ambayo yanaweza kuuzima moto huo ambao Mungu amewasha. Kwa maana ni kusudi la Mungu kwamba nuru Yake ya uhuru iwakayo itawaka hadi Kuja kwa Bwana, na hakuna mamlaka inayoweza kuizima. Wataifanya kuwaka zaidi kadri wanavyopuliza. Imethibitishwa kupitia vizazi kwamba mateso huliimarisha Kanisa.

43 Naye Danieli, bila kujua jinsi Mungu atakavyofanya jambo hilo, na bila kujua kama Mungu alikuwa anaenda kufanya jambo hilo, bali akijua ya kwamba Yeye aliweza, pia, kufanya jambo hilo, na akijua ya kwamba kitu fulani ndani yake kilimwambia hivyo. Unaona, Mungu alikuwa na kusudi. Alikuwa na kila kitu kikifanya kazi kwa kusudi hilo.

44 Na wote, leo, haijalishi tunaonekana kutojali wakati mwingine, na jinsi mambo yanavyoenda kiajabu, na jinsi Kanisa linavyoingia katika hali *hii* na hali *hiyo*, yote ni kusudi la Kiungu la Mungu kutufinyanga na kutufanya katika njia Yake Mwenyewe. Ni nani anayejua jinsi ya kutengeneza nyenzo zaidi ya Muumba?

45 Na simba hawakuweza kumla nabii, kwa sababu Mungu alimtuma Malaika. Alikuwa na Malaika aliyesimama pale kumlinda nabii huyu, kwa sababu Mungu alikuwa na kusudi. Alitaka kumwonyesha yule aliyejifanya mfalme mkono Wake wenye nguvu na kusudi Lake.

46 Nafikiri hicho ndicho kinachoendelea leo, kwamba Mungu anatayarisha watu, ili aweze kuonyesha mkono Wake wenye nguvu, ili kutimiza kusudi Lake kuu. Loo, nina furaha sana, asubuhi ya leo, kwamba Yeye anaishi moyoni mwangu, ya kwamba Yeye si Mungu mfu. Yeye ni Mungu aliye hai. Na chini kabisa ndani yangu . . .

47 Jana asubuhi, nilikuwa nimeketi kwenye kiti cha kinyozi, ili kunyolewa. Kijana mmoja alikuwa akininyoa nywele, kule chini kwenye duka la Ndugu Egan. Nami nilikuwa nimeketi tu pale, nimeinamisha kichwa changu. Na, loo, nimekuwa na uchovu sana. Mikutano yangu imekuwa mirefu sana, na ninajaribu kuondoka, asubuhi, kwa mapumziko kidogo kabla ya ibada hizi zinazofuata kuanza. Na nilikuwa nimechoka sana, ilionekana tu kama moyo wangu ungeacha kupiga. Na nilipokuwa nimeketi pale, mara ghafula, niliweza kusikia kila mtu akizungumza, lakini ilionekana kana kwamba nilikuwa nje angani.

48 Nikawazia, “Je, nimepata mshtuko wa moyo, na ninaondoka kwenye kiti hiki cha kinyozi?” Nikawazia, “Nashangaa kama hicho ndicho kinafanyika?” Nikagusa mikono yangu; ilikuwa imekufa ganzi. Na moyo wangu ulionekana kama umeacha kupiga. Na nikawaza, “Loo, lakini kuna Injili inayopaswa

kuhubiriwa. Na hakuna nguvu inayoweza kunichukua hadi kusudi la Mungu litimie."

49 Hakuna kitu kinachoweza kunidhuru, hata kidogo, hadi kusudi la Mungu litimie. Na hilo litakapotimia, ninataka kwenda na kusudi Lake. Wakati Yeye amemaliza, basi nimemaliza, pia. Anapomaliza na mimi, nimemalizana na maisha.

50 Wakati Yeye amemaliza na wewe, wewe umekwisha, pia. Kwa hivyo inaleta tofauti gani? Mungu anayashikilia yote mkononi Mwake. Tuwe vijana au wazee, hatujui ni lini kusudi la Mungu litatimia na kukamilika. Mungu huwachukua watoto wachanga, wakati mwingine, kuonyesha ya kwamba anaweza kuongoza nafsi zao ndogo. Kila kitu afanyacho Yeye ni kwa kusudi. Alisema, hata shomoro hawezi kuanguka kutoka mbinguni, bila Yeye kujua. Kila kitu kinakwenda kwa kusudi Lake, kwa saa tu na kwa wakati. Yote yako katika mpango Wake wa Kiungu. Hakuna kinachoweza kuharibu.

51 Jinsi ilivyokuwa hakikisho kwa Ibrahimu, baada ya kumpata Mungu, na kujua ya kwamba Mungu alikuwa na kusudi. Kwamba, katika kusudi hili, Yeye alikuwa anaenda kuleta, kupitia kwa Ibrahimu na Sara, mwana. Na kupitia mwana huyu, Isaka, alikuwa anaenda kuja Bwana Yesu. Na katika kusudi hili, alikuwa akiwaleta Sara na Ibrahimu, na alikuwa anaenda kuwafanya watu wakuu na kumleta mwana huyu; kuchukua watu wabaya sana ambao wanaweza kuwepo, kulifanya nao.

52 Ni ajabu jinsi gani, kwamba Mungu anatembea kwa njia za ajabu! Vema, ilionekana kana kwamba, kama angetaka kumleta mtoto, kwa ulimwengu namna hiyo, angeweza kuchukua mwanamke ambaye alikuwa na uzazi. Ilionekana kana kwamba angemchukua mtu ambaye hakuwa tasa. Kama Ibrahamu na Sara, walikuwa wameoana kwa miaka mingi, mingi sana, na hakuwa na uwezo wa kuzaa. Hakuweza kuzaa mtoto. Vema, ilionekana kana kwamba, basi, Yeye angemchukua mwanamke mchanga ambaye alikuwa na rutuba, ambaye angeweza kumzaa mtoto huyu. Lakini Mungu anapenda kuonyesha neema Yake. Mungu anapenda kuchukua kitu ambacho si kitu na kutengeneza kitu kutokana nacho, kwa maana Yeye ni Muumba.

53 Hiyo ndiyo sababu alikuchukua wewe na mimi. Sisi hatukuwa kitu, ili aweze kutufanya watoto Wake Mwenyewe, kutoka kwetu sisi tuliokuwa wanyonge, na wenye mashaka, na waliopotea, na vipofu, na wasiopendeza, kutufanya kuwa watoto Wake wapendwa. Ni kusudi la Mungu kufanya hivyo.

54 Na halafu, tena, ilionekana kana kwamba Mungu angalimchukua mwanamke kijana na mwanamume kijana, kufanya hili, mwanamke kijana na kijana mwanamume ambao walikuwa ndiyo kwanza wamefunga ndoa. Angesema, "Sasa,

hujapata watoto. Nami nitakufanya wewe, mwana wako wa kwanza kuzaliwa, nami nitafanya . . . Atakuwa Isaka Wangu."

55 Lakini Mungu alichagua mwanamume mwenye umri wa miaka sabini na mitano, na mwanamke mwenye umri wa miaka sitini na mitano, ili afanye kusudi Lake, ili kuonyesha kwamba unaweza kuwa kijana au mzee, Mungu bado anaweza, na atafanya, kutimiza kusudi Lake. Hakika. Na wakati Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka sabini na tano, alipata ahadi ya Mungu. Akamwambia Sara.

56 Na sasa ibilisi akasema, "Unajua nini? Nitachelewesha tu hilo kwa muda. Ninaamini ikiwa nitawafanya wazeeke sana, watapoteza imani, na watajua kwamba haiwezi kutukia. Ikiwa tayari wanatetemeka kwenye miaka sabini na tano; ikiwa naweza tu kuiweka mbali kwa muda!" Naye akaizuia mpaka Ibrahimu na Sara walikuwa wameinama katika uzee, mvi na mabega yaliyoinama.

57 Inaonyesha tu kwamba hakuna kitu kinachoweza kushinda kusudi Lake. Hata kifo hakiwezi kushinda kusudi Lake. "Ibrahimu alikuwa sawasawa na mfu." Na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa kwa miaka arobaini au hamsini, lakini hakuna kitu kinachoweza kushinda kusudi la Mungu. Mwili wake ulikuwa mzee; ulikuwa umekunjamana; mishipa ya maziwa ilikuwa imekauka. Moyo wake ulikuwa dhaifu sana asingeweza kupitia utungu wa kuzaa. Lakini Mungu alitujulisha hapo, kwamba kusudi Lake halitashindwa. Alimbadilisha Sara, na kumfanya msichana tena. Ndipo akamchukua mwanaume, mwenye umri wa miaka mia moja, na kumrudisha kwenye ujana wake.

58 Hata ionekane isiyo ya kimantiki jinsi gani, Mungu alitoa ahadi hiyo. "Wala Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu, kwa maana alimchukulia, ya kwamba Yeye aweza kufanya yale aliyoahidi."

59 Basi tunapaswa kuwa nini asubuhi ya leo? "Sisi ni watoto wa ahadi Yake. Sisi tukiwa wafu katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja Naye, pamoja na ahadi." Basi, haidhuru ni magonjwa kiasi gani yanakuja, tunakufa kifo cha namna gani, tunapitia umaskini kiasi gani, kusudi la Mungu haliwezi kushindwa. Atatuinua tena. "Kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtaishi." Hilo ndilo tumaini letu.

60 Ninapojua, leo, ikiwa ni siku yangu ya kuzaliwa, na ninapata kuwa mzee. Ninajiangalia kwenye kioo na ninaona kwamba mvulana huyo mdogo, aliyejenga maskani hii, si yule mvulana mdogo tena. Anakuwa mzee, mabega yanainama, ndevu zinabadilika kuwa mvi, nywele zinatoka, lakini hakuna kitu kinachoweza kulishinda kusudi la Mungu. Hakuna kinachoweza! Kwa hiyo naitumainia ahadi, "Kwa kuwa mimi ni

hai, ninyi nanyi mtaishi." Ninaungana na Ayubu wa kale, "Najua mkombozi wangu yu hai, na siku ya mwisho atasimama juu ya nchi." Ni kusudi alilo nalo Mungu. Lazima nitimize kusudi hili. Maisha yangu yote lazima yaletwe katika kusudi Lake, na kwa mpango Wake. Kila mmoja wetu yuko hivyo. Mungu ana kusudi ambapo . . .

61 Mzee Ibrahimu angeweza—angeweza kustahimili, kama kumwona Yeye asiyeonekana, kwa sababu lilikuwa kusudi la Mungu, kwamba ajue kwamba Mungu alimpa ahadi. Hiyo, haidhuru jinsi kila kitu kilionekana kuwa kinyume, Mungu alimpa Ibrahimu ahadi hiyo. Kwa hiyo, Mungu alitimiza ahadi Yake. Alilitimiza, kwa Ibrahimu. Alilitimiza, kwa watoto Wake wote. Na atatimiza ahadi Yake.

62 Ilikuwa ni Musa, alipofundishwa hekima yote ya Wamisri, alipojua kwamba Mungu alikuwa na kusudi kwa maisha yake.

63 Ilikuwa ni Yokebedi, mama yake, ambaye alimchukua mtoto wake mpendwa, mtoto mzuri zaidi katika ulimwengu wote, wakati huo, maskini mtoto mzuri; akamweka ndani ya safina, akamsukumia nje ndani ya mto Nile, ambapo mamba walikuwa wamenona kutokana na watoto wadogo wa Kiebrania, maana walikuwa wakiwalisha mamba. Naye akamchukua mtoto wake mchanga na kumsukuma nje kwenye taya za kifo, akijua hili, kwamba kusudi la Mungu haliwezi kushindwa. "Mungu wa Ibrahimu, mtunze mtoto wangu, na umlete kwenye kusudi ambalo umemletea." Hakukuwa na maji ya kutosha katika Nile kumzamisha. Hakukuwa na mamba wa kutosha katika ulimwengu wote ambao wangeweza kummeza. Alikuwa mteule wa Mungu.

64 Na kama alivyokuwa mteule wa Mungu, kwa kusudi hilo, sisi ni wateule wa Mungu leo, ambao tunaamini katika ufufuo wa Bwana Yesu. Na hakuna mabomu, hakuna kuzimu, hakuna kitu kingine chochote kinachoweza kuharibu kusudi la Mungu. Hatuna budi kwenda katika ufufuo. Ni ahadi tuliyo nayo kutoka kwa Mungu. Kusudi la Mungu.

65 Na, Musa, alipofikia umri wa miaka arobaini kamili, mtu wa makamo, naye alikuwa amefunzwa shuleni. Lakini Mungu ana njia ngumu sana, wakati mwingine, ya kutimiza mambo Yake, ambayo ameahidi. Jinsi alivyomrudisha Musa nyuma ya jangwa, na kumwacha asikie mayowe na vilio, alipokuwa akiyumbayumba nyikani. Na akiwa huko nyuma, peke yake katika majangwa, na pepo zikivuma, nge na nyoka, na, peke yake, huko nyikani, hata karibu aangamie. Hakuna chochote kinachoweza kushinda kusudi la Mungu. Mungu alikuwa amemleta Musa, na Musa ilimbidi kufanya kile ambacho Mungu alimwambia afanye, maana kusudi la Mungu haliwezi kushindwa.

66 Ilikuwa ni mhusika wetu, asubuhi ya leo, Ayubu, ambaye alipokuwa katika dhiki kuu sana, wakati utajiri wake wote ulikuwa umeondoka kwake. Watoto wake walikuwa wamekufa. Mwili wake ulitokwa na majipu. Naye alikuwa katika dhiki kuu sana ambayo alipata kuwa nayo. Akiwa ameketi juu ya lundo la majivu, akiwa na kigae, akikwaruza majipu. Na mkewe mlangoni, "Kwa nini usimlaani Mungu na ufe?"

67 Wakati washiriki wa kanisa lake walikuwa wamemgeuzia migongo yao, kwa siku saba, na kumshtaki. Wakati, walipaswa kuwa wakimfariji. Lakini walikuwa wakimshtaki kuwa mtenda dhambi wa siri, wakimshtaki kuwa ni mwasi.

68 Ilikuwa ni katika saa ile kuu, ilikuwa katika wakati huo mkuu, ulikuwa ni wakati ambapo Mungu alimpeleka Ayubu kwenye mchanga mtakatifu; ambapo humpeleka kila mwaminio, kwenye tukio, hadi upande wa nyuma ya jangwa, kama alivyomfanyia Musa; mpaka kwenye chumba kidogo cha faragha, ambako alikupeleka; mpaka kwenye kibanda cha makaa ya mawe, nilipoupokea. Mungu ana mahali, na kusudi, na wakati. Na wakati alipokuwa na Ayubu katika hali hii, alimweka kwenye mchanga mtakatifu, kwa maana Yeye alikuwa anaenda kumfunulia jambo fulani, ambalo halingeondoka kamwe.

69 Loo, kwa mchanga huo mtakatifu! Hana budi kumpeleka kila mtoto wa kweli huko. Anakupeleka kwenye sehemu hizo, ambapo hakuna ibilisi awezaye kuja. Hakuna mwalimu anayeweza kuelezea jambo Hilo vinginevyo. Anakupa kitu fulani kwenye mchanga huo kule nyuma, kile cha uzoefu, ambacho hutasahau kamwe mradi nyakati zinasonga; haijalishi mama yako, baba yako, mume wako, mke wako, washirika wako wanaweza kuwa watu wakana-mungu kiasi gani. Kila mwaminio wa kweli ana mahali pale ambapo Mungu amekutana naye. Hakuna aliyeachwa nje. Kila mwaminio anapo. Kila mtu aliyezaliwa kwa Ufalme wa Mungu anajua mahali hapo, dakika hiyo, saa ile ambapo Mungu alimchukua. Na juu ya mchanga huo mtakatifu, katika Uwepo wa kichaka kilichowaka moto, Yeye alifanya jambo fulani kwa mwaminio huyo, hata mawazo yote ya ulimwengu hayangeweza kuharibu. "Juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayataliharibu." Juu ya Mwamba huu, ufunuo wa kiroho wa Yesu aliyefufuka! Juu ya Mwamba huu!

70 Ayubu, katika dhiki yake, kila kitu kilitoweka. Mke wake alikuwa amemgeuka, na alikuwa akimshtaki. Na marafiki zake wote waaminio walikuwa wamemgeuka kwa sababu walikuwa na theolojia tu. Na wengine wote walikuwa wamemgeuka.

71 Lakini Mungu alisema, "Njoo hapa, Ayubu. Nitakupa kitu, jamani. Nitaweka ndani yako kitu ambacho ibilisi wote wa kuzimu hawawezi kukitikisa." Na katika. . . Kila mwalimu

ulimwenguni anaweza kukushtaki kwa njia moja au nyingine, lakini hakitasonga kamwe. Unajua alifanya nini? Aliinua pazia kidogo tu, na kusema, "Ayubu, tazama kule!" Naye Ayubu aliona nini? Unafikiri aliona nini? Aliiona Pasaka, kwa mara yake ya kwanza. Aliona Pasaka ya kwanza, akapiga kelele, "Najua Mkombozi wangu yu hai!"

72 Loo, mahali penye baraka jinsi gani kuwepo! Kila mwanamume aliyechaguliwa na Mungu, na kila mwanamke na mtoto, hufika mahali hapo kwenye mchanga huo mtakatifu, kufikia ambapo Mungu huinua pazia na unamwona katika uweza Wake uliofufuka. Unajua ya kwamba Yu hai. Na sisi, kama Ayubu, tunaweza kulia, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu wa ngozi waharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili huu nitamwona Mungu."

73 Mtazamo huo wa kwanza wa Pasaka ulimfanya nabii apige mayowe. Na ngurumo zikavuma, na radi zikamulika. Aliona Pasaka, mara yake ya kwanza. Aliiona lini? Sio alipokuwa amevaa nguo zake zilizopambwa vizuri; si wakati alikuwa amechana nywele zake, pengine, vizuri kabisa; si wakati alipokuwa akifurahia afya bora kabisa. Lakini alipokuwa katika shida, alipokuwa amelala katika shida, kwenye saa hiyo, na karibu kufa kwake, ndipo alipoiona Pasaka. Hapo ndipo alipoona ufufuo wa kwanza.

74 Loo, imekuwa sawa na mimi na wewe. Imekuwa wakati tulipolala madhabahuni, mahali fulani, mpaka tulipokuwa tayari kufa, na kusema, "Bwana Mungu, nifanyie kitu!" Hapo ndipo Mungu alipoinua pazia na tukaiona Pasaka.

75 Tunaona Pasaka, sio kwa njia ya theolojia, sana. Hatujawahi kuona Pasaka, kama kuvaa nguo mpya. Hatujawahi kuona Pasaka, kama sungura wadogo na mayai yaliyopakwa rangi. Tunaiona Pasaka katika uwezo wa ufufuo wa Bwana Yesu Kristo. Hiyo ilikuwa Pasaka halisi.

Na alipopiga mayowe, Mungu akajibu kwa Moto.

76 Ilikuwa ni Daudi alipokataliwa na kuhamishwa. Ilikuwa ni Daudi, baada ya kutenda dhambi na kufanya uhalifu huo wa kutisha. Ilikuwa ni Daudi alipokuwa amechanganyikiwa na mtoto wake kuchukuliwa, furaha ya moyo wake. Ilikuwa ni Daudi, nabii na mfalme, ndiye aliyelia alipoona ya kuwa alikuwa anazeeka, naye lazima arudi kwenye mavumbi ya nchi. Daudi ndiye aliyesema, "Zaidi ya hayo, mwili wangu utakaa katika tumaini, kwa maana hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu, wala hataiacha nafsi Yake katika kuzimu."

77 Ilikuwa wakati Daudi alikuwa na wakati wake mbaya zaidi. Ilikuwa wakati Daudi alifadhaika na kuhangaika, na saa ile ile ya kufa, karibu, kwamba wakati Mungu aliinua pazia, akasema, "Angalia kule, Daudi!"

78 Daudi akasema, “Mwili wangu utatulia katika tumaini, kwa maana hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu. Wala hataiacha nafsi Yake kuzimu, hivyo mwili wangu utatulia katika tumaini.”

79 Loo, ni saa hiyo, rafiki. Ni wakati huo. Ni katika saa hizo muhimu, za kusulubiwa ndipo tunapoona ufufuo. Ni katika wakati huo, ambapo Mungu anapenda kuonyesha neema Yake. Ni katika wakati huo ambapo Mungu anapenda kuwafariji watoto Wake.

80 Saa ya giza kuu kuliko yote ambayo ulimwengu huu umewahi kuona ilikuwa Ijumaa Kuu; wakati matumaini yote, yote yaliyoandikwa, matumaini yote waliyokuwa nayo yalikuwa yale yaliyoandikwa kwenye karatasi. Matumaini yote waliyokuwa nayo ni yale ambayo mwanafalsafa fulani alikuwa amesema, na huyo hapo Mkuu wa Uzima akifa pale Kalvari. Ilikuwa saa yenye giza zaidi kuwahi kutokea duniani.

81 Lakini Pasaka ilitoa saa angavu zaidi ambayo ulimwengu umewahi kuona, kwa sababu ushirikina wote na mashaka yote na hofu zote ziliondolewa Mungu alipomfufua.

Kwa nini kulikuwa na giza? Ni nini kinachofanya iwe giza?

82 Hebu tufuate, kama nilivyosema muda mfupi uliopita, kuhusu ndege, kuhusu maua. Kuhusu, kwa nini maua madogo ya Pasaka huchanua kwenye Pasaka? Kwa nini ndege huimba katika majira ya kuchipua katika mwaka? Kwa nini maua huchanua? Ni kwa sababu inakuja majira ya joto. Ni nini hufanya hivyo? Mnamo Februari, karibu mwezi mbaya zaidi tuliokuwa nao, majira ya baridi kali yamekuwa yanaendelea, yanaendelea, yanaendelea, yanaendelea, mpaka yanapogonga mara yake ya mwisho, ndipo yanarudi nyuma, kufungua njia kwa ajili ya uhai. Kifo kimeleta pigo lake la mwisho. Ni lazima kirudi nyuma na kuachilia uhai kuchukua mahali pake.

83 Ni nini hufanya giza kabla ya mchana? Ni giza zaidi kabla ya mapambazuko. Tunaambiwa, na wanasayansi, kwamba ni nuru inayosukuma, ikija, ikishuka chini. Jua linakuja kote ulimwenguni. Nuru yake inasukuma giza. Linatoa pigo lake la mwisho. Hawezi kusimama tena. Giza haliwezi kamwe kusimama mbele ya mwanga. Haliwezi kusimama. Nuru ina nguvu mara milioni kumi kuliko giza, hivyo nuru na giza haviwezi kukaa pamoja. Na nuru inapoanza kuchomoza, giza hutulia na kuwa nene. Inalifinyilia pamoja.

84 Kama vile kudondosha wino kwenye be—beseni iliyojaa sabuni. Hauko tena. Hakuna weusi tena wa wino unapodondoshwa kwenye sabuni. Inakuwa sabuni, yenyewe.

85 Loo, hivyo ndivyo dhambi ilivyo. Wakati inapodondoshwa kwenye Damu ya Mwokozi, haiko tena. Imetoweka. Si ajabu alisema, “Iko katika bahari ya usahaulifu.” Beseni ya sabuni ya Mungu ambayo haiwezi kupatikana tena. Inasambaratika tu.

Haipo tena. Hivyo ndivyo dhambi ilivyo, mara unapoona ufufuo halisi na gharama ambayo ililipwa kwa ajili ya ufufuo huo.

86 Giza, linaganda pamoja, kwa sababu hivi karibuni litatoweka. Na mara tu nuru inapokuja, giza halipo tena. Je, linaenda wapi? Ni nini kilitukia kwa usiku ule mweusi, saa chache zilizopita, ulioning'inia kwenye maskani hii? Hauwezi kuwepo sasa. Jua linawaka. Ulienda wapi? Uliinua sehemu gani, au ulishuka kwenda wapi? Haukuwapo tena. Na sababu kulikuwa giza, ni kwa sababu hapakuwa na mwanga.

87 Na sababu ya kwamba mwanadamu hakuwa na tumaini, hapakuwa na ufufuo. Lakini Pasaka ilileta ufufuo. Sasa giza halipo tena. Ni Nuru.

> Tutatembea katika Nuru hii, Nuru hii nzuri,
> Ambayo huja pale ambapo matone ya umande
> wa rehema yanang'aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

88 Usiku unaendelea, na tuweke hilo sasa kitaifa. Hii ndiyo saa ya giza zaidi, saa ya giza zaidi ambayo ulimwengu huu umewahi kuona. Hata maumbile hutetemeka. Wakati mmoja, dunia hii yote inaweza kuwa unga. Nini kitatokea kwa majibu. . .na majibu ya haidrojeni au—au—au oksijeni, au baadhi ya mabomu haya makubwa, majibu ya atomiki? Kila mti, kila unyasi, kila kitu, kila kiungo, kila kusudi, kila mtu, kila kitu, kingevunjika vipande vipande na kugeuka kuwa asidi. Unaona ni nini? Dunia nzima inatetemeka. Kuna mabomu tayari.

89 Kila kitu kinaonekana kuwa kimewekwa sawa kwa wakati. Na ikiwa giza limewekewa wakati wake, ni zaidi sana vipi Nuru imewekewa wake!

90 Ni nini kinachofanya kuwe giza sasa? Ni nini kinachofanya mambo haya? Makanisa yote yanatengana. Tunabishana. "Loo, ni huko? Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni Church of God. Mimi ni Assemblies." Loo, hamwezi kuona, enyi watoto? Ikiwa hiyo ndiyo tu tuliyopaswa kusimamia, tungekuwa watu duni zaidi ulimwenguni.

91 Nina furaha sana kwa ajili ya mahali padogo, patakatifu, mahali padogo hapa chini kwenye Barabara kuu ya Ohio, katika kibanda cha makaa, usiku mmoja, ambapo Mungu aliinua pazia. Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Wapentekoste, wote walitoweka wakati huo, kwa maana niliiona Pasaka. Nilimwona Yesu kama Mwokozi wangu. Nilimwona kama ufufuo na Uzima. "Yeye aniaminiye Mimi—Mimi, ijapokuwa amekufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Ninamwona kama Mfalme pekee na Mtawala, kitu pekee ambacho kingeweza kunisaidia, Mpaji pekee wa Uzima wa Milele, Yeye pekee ambaye angeweza kuponya ugonjwa wangu, angeweza kuondoa magonjwa yangu, ambaye angeweza

kunifufua katika siku za mwisho. Aliniacha tu niangalie ng'ambo ya pazia, nami nikamwona Yeye, ufufuo. Kisha nikaungana na Ayubu, "Najua Mkombozi wangu yu hai!" Na baada ya kutokuwapo tena na Mmethodisti, au Mbaptisti, au Mpresbiteri, au Wapentekoste, Mkombozi wangu bado ataishi kwa hali hiyo hiyo.

92 Unaweza kusema, "Vema, hii ni *hivi*, na hiyo ni *hivyo*; isipokuwa ufanye *hivi*, isipokuwa ufanye *vile*."

93 Ninajua vizuri zaidi, kwa sababu nimetazama ng'ambo ya pazia la wakati. Nimekuwa kwenye mchanga mtakatifu; pamoja na kila mwaminio hapa ndani. Hakuna ibilisi awezaye kugusa mchanga huo. Hakuna daktari wa theolojia anayeweza kuuondolea mbali kwa maelezo. Aliniponya nilipokuwa mgonjwa. Aliniokoa nilipokuwa nimepotea. Anaishi milele. "Uniulize ninavyojua kuwa Yu hai? Anaishi ndani ya moyo wangu."

Hajafa, bali amefufuka kutoka kwa wafu.

94 Na giza hili kuu linatanda juu ya dunia sasa, si kitu ila kutangaza ya kwamba Nuru inasonga chini.

95 Wakati kifo kinaning'inia karibu sana, hata inaweza kuwa katika saa moja. Katika saa moja kutoka sasa, dunia inaweza kukutana na kifo chake. Ikiwa kifo kinaning'inia karibu hivyo, kinafanya nini? Ni Uzima, Uzima unakuja; ufufuo, Pasaka kwa watoto wote wa Mungu. Inaning'inia chini. Inasukuma. Malaika wanashuka. Roho Mtakatifu mkuu anaingia ndani. Giza linachukua hatua yake ya mwisho, kwa kuwa Nuru itakuwa hapa hivi karibuni. Kristo atakuja, furaha na tumaini la nyakati, ufufuo wa kweli kwa waaminio wote. Kwa maana tutashiriki pamoja Naye katika ufufuo Wake, kama tulivyoshiriki Naye katika mateso Yake. "Anayeteseka pamoja Nami atatawala pamoja Nami."

> Loo, basi, lazima nipelekwe Nyumbani hadi Mbinguni
> Katika kitanda kizuri cha starehe,
> Wakati wengine walipigana wapate kushinda tuzo,
> Na kusafiri kwa bahari ya umwagaji damu?
>
> Hapana, lazima nipigane ikiwa lazima nitawale.
> Niongezee ujasiri, Bwana.

96 Hayo ndiyo maombi yangu. Loo, ni lazima nisiende kama mwoga. Sipaswi kuzunguka, kila siku, na kichwa changu kikining'inia chini, kana kwamba kuna kitu kibaya. Ninapoutazama ulimwengu na giza lake lote, na matendo yao yote; lazima niinue kichwa changu, nitembee na kichwa changu kati ya tai, nikijua hili, kwamba, "Ninamjua katika uwezo wa ufufuo Wake." Kwa sababu anaishi, sisi pia tunaishi. Kwa

sababu alifufuka kutoka kwa wafu, nami nitafufuka. Wewe pia utafufuka. Hiyo ndiyo maana ya Pasaka kwa mwaminio.

97 Wakati fulani uliopita, huko katika... Vita vya Kwanza vya Dunia vilikuwa vinaendelea. Walikuwa na gesi kubwa walizotupa, kama vile gesi ya haradali na klorini, na ilikuwa hatari. Ingetia sumu kila kitu. Majani yangekufa, miti ingekufa, na nyasi zingekufa, kila kitu, ambapo gesi hiyo (hiyo gesi ya haradali) ingeiteketeza wakiitupa.

98 Kasisi, asubuhi moja ya Pasaka, alikuwa akishuka kupitia ma—mahema walipokuwa wamelala waliojeruhiwa na waliokuwa wakifa.

99 Muuguzi wa Msalaba Mwekundu akaja. Wavulana hao walikuwa wamekaa mbele kwa muda mrefu sana, huko nje, walikuwa wamechoka sana. Na kwa hivyo alikuwa na lu—lundo la waridi mkononi mwake, na alipokuwa akipita karibu na kila kitanda kidogo ambapo wavulana walikuwa wamelala, akilia. Ilikuwa Pasaka. Pasaka iliyoje kwao; ndege zilikuwa zikiruka, na mabomu yakianguka! Angeweza kuchukua waridi na kumpa kila mvulana, aseme, "Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu." Askari hao wangeshika waridi na kupiga mayowe, kwa maana walijua ya kwamba waridi hilo lilikuzwa katika nchi yao.

100 Ndugu, asubuhi ya leo, tuko katika ulimwengu wa gesi hatari za sumu. Tuko katika ulimwengu ambapo kila aina ya mafundisho na kadhalika, inayosema, "Hakuna ufufuo. Na hakuna uponyaji wa Kiungu. Hakuna *hiki*, au *kile*, au *kinginecho*." Lakini, si muuguzi wa Msalaba Mwekundu; lakini Roho Mtakatifu anakuja, mara moja moja, na kutuleta juu ya mchanga huo mtakatifu wa neema ya Mungu, na kumwaga ndani ya mioyo yetu ishara kidogo kutoka Nchi iliyo ng'ambo ya mto.

101 Alisema, "Mhubiri, rafiki," akasema, "Nilisimama pale na kulia, mpaka nikawa nalia sana, hata nikasema... Mmoja wa wavulana alikuwa akienda kwa pikipiki, huko kwenye mstari wa mbele, kupita La Salle, Lorraine, na alisema alikuwa anaenda huko kufanya aina fulani ya u—upelelezi. Na akasema... Nikamwambia, 'Sajenti, naweza kupanda na wewe?' Akasema, 'Hakika, kasisi, ingia ndani mara moja.' Akasema, 'Unachukua ninii yako mwenyewe...' Kasema, 'Hiyo ni sawa. Ningependa tu kupanda gari pamoja nawe.' Kasema, 'Bila shaka, ingia ndani mara moja.'"

102 Akasema, "Tuliendesha gari hadi tukafika kwenye jangwa lile lililokuwa limepauka, ambako hakukuwa hata na chembe ya unyasi wala chochote." Na akasema, "Alipokuwa akipanga nyenzo zake, kwamba alipaswa kurudisha ujumbe, ama chochote alichopaswa kufanya," alisema, "Nilizunguka pale kidogo. Nikawazia, 'Loo, hii si ni Pasaka! Nje katika nchi hii, ambapo mabomu yameangusha majengo yote chini, ambapo miti inaangushwa, kwa risasi za bunduki ya marisau, hakuna

hata chembe ya unyasi iliyobaki.'" Akasema, "Ee Mungu, hii ni picha ya ulimwengu huu, baadhi ya siku hizi, wakati dhambi imeushika. Hii itakuwa ndiyo picha."

103 Na akasema, "A—akili yangu na macho yangu yalivutiwa na mwamba fulani." Na akasema, "Nilikwenda huko, nikafikiria, 'Bwana, kwa nini wataka nisimame karibu na mwamba huu?'" Akasema, "Niliinua tu jiwe juu, na, nilipofanya hivyo, yungiyungi dogo la Pasaka lilikuwa limeinua kichwa chake. Lilikuwa limelindwa wakati wote wa dhoruba. Katika gesi zote za sumu, hazijawahi kulisumbua, kwa kuwa lilikuwa limefichwa kwenye mwamba."

104 "Najua Mkombozi wangu yu hai." Ee Mungu, bila kujali ulimwengu unasema nini, unifiche katika Mwamba wa Miaka, Bwana. Dhoruba zikipita, wacha niinue kichwa changu tena. Kwa sababu anaishi, sisi pia tunaishi. Mwaminio anaweza kusema nini, ambaye amekuwa kwenye mchanga, ambaye ameshuhudia mambo haya? "Najua Mkombozi wangu yu hai."

105 Kanisa, ulimwengu, ninii. . . anaenda kanisani asubuhi ya leo; wengi wao, ili kuonyesha koti jipya; baadhi yao, ili kuonyesha kofia mpya. Hawatawaona tena hadi Pasaka ijayo tena. Ni kwenda kwa ajili ya maonyesho ya ulimwengu na ubatili. Wengi wao wanaenda kanisani, ili tu kujificha nyuma ya dhambi zao na kuwa wa madhehebu fulani makubwa, na kusema, "Mimi ni *Fulani-wa-fulani*. Mimi ni wa *Fulani-wa-fulani*." Hayo ndiyo yote wajuayo. Hayo ndiyo yote waliyoamini.

106 Lakini, loo, kwetu, asubuhi ya leo, kwa neema ya Mungu, tumesimama mahali ambapo Musa alisimama; tulisimama mahali ambapo Ayubu alisimama; tukasimama mahali aliposimama Daudi; na tunapiga kelele kwa sauti yetu yote, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya dunia hii; ijapokuwa mabuu wa ngozi wauharibu mwili huu, hata hivyo, katika mwili wangu nitamwona Mungu, ambaye nitamwona mimi mwenyewe; macho yangu yatamtazama, wala si mwingine. Hatukuleta chochote katika dunia hii; ni ubatili na kiburi. Ni hakika hatutoi chochote. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana lihimidiwe." Jambo moja alilojua, "Mkombozi wangu yu hai!" Si, "*Ataishi*." "Anaishi," huo ni mwendeleo wa milele. "Anaishi!" Na kwa sababu. . . Yesu alisema, "Kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mnaishi."

107 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo sasa, kwa maombi ya kufunga.

108 Loo, leo, maskini rafiki yangu duni, ikiwa hujawahi kufika mahali hapa! Loo, unasema, "Nimekuwa hapa maskanini, mara nyingi, Ndugu Branham." Hiyo ni nzuri sana. Ninathamini hiyo. "Loo, nimekuwa kwenye makanisa mengine. Nimesikia

wahudumu hodari wakizungumza." Hiyo ni nzuri sana. "Ninasoma Biblia yangu." Hiyo bado ni sawa.

109 Lakini je, umewahi kufika mahali pale ambapo Yeye ameinua pazia, mahali pale patakatifu ambapo tukio liligusa moyo wako; hata unajua Pasaka haikuwa hadithi fulani ya uwongo; hata unajua Pasaka haikuwa Santa Claus, kitu fulani kidogo cha kubuni; hata unajua mwenyewe kwamba Yu hai; na kwa kuwa Yeye yu hai, wewe pia unaishi? Kama hujawahi kupitia jambo hilo, huu ndio wakati mzuri zaidi, ulimwenguni, kumwacha Mungu ainue pazia, asubuhi ya leo. Yesu yu hai. Amefunguliwa, duniani, asubuhi ya leo. Yeye ni Mwokozi wako leo; anaweza kuwa Hakimu wako kesho.

110 Lakini hivi hujawahi kukutana na tukio hilo? Kama sivyo, je, waweza kuinua tu mkono wako, na kusema, "Mungu, unirehemu. Sasa nitaamini"? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . mtu kule nyuma, kwa mkono wake. Mungu akubariki, bwana, huko. Mtu mwingine inua mikono yako.

111 Wote humu ndani sasa, ambao hawajapata tukio hilo, naomba uinue mkono wako, useme, "Mungu, asubuhi ya leo, kwa njia Yako mwenyewe ya Kiungu . . . Sikuombi Wewe wala sikuambii jinsi yakupasa kunipa, Bwana. Lakini, kwa njia Yako mwenyewe ya Kiungu, Bwana, utanipeleka mpaka mahali pale ambapo jambo fulani litatendeka moyoni mwangu? Nimekuwa na mema na mabaya, nikienda huku na huku, na siwezi tu kutulia, kwa njia fulani. Lakini acha hii iwe Pasaka halisi kwangu. Nipeleke mahali pale, Bwana, nyuma ya jangwa. Hapo uufinyange moyo wangu, sasa hivi. Na unipe mchanga huo mtakatifu nisimame, mahali ambapo hakuna pepo, wala kitu kingine chochote, wala mtu yeyote kuwahi kuniambia chochote, najua ni halisi. Acha niangalie kupita pazia la wakati, kwa ajili ya kesho. Hiyo ndiyo sababu nimekuja hapa, asubuhi ya leo, Bwana, kupata jambo hilo. Nimemsikia mhubiri akijaribu kueleza. Nataka unifunulie."

112 Je, unaweza kuinua mkono wako? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, na wewe huko nyuma, huyo kijana. Na Mungu awe nawe. Upande wangu wa kushoto hapa, kwenye marefu ya kushoto. Upande wangu wa kushoto, mtu yeyote angesema, "Mungu, unirehemu, sasa hivi." Mungu akubariki, hapa katika marefu haya mengine. Ndiyo. Inua mkono wako, useme, "Mungu, unirehemu." Mungu akubariki, msichana.

Ninatamani nyumbani na nimechoka, na ninataka kumwona Yesu,
Ninataka kusikia kengele tamu za bandari zikilia;
Ingeangaza njia yangu na ingeondoa hofu zote;
Bwana, nijalie nitazame nyuma ya pazia la wakati.

113 "Hebu niangalie kidogo tu, nimwone Yesu katika ufufuo Wake." Je, kunaweza kukawa mwingine kabla ya kufunga katika maombi sasa? Kuwa mwaminifu tu. Inua mkono wako. "Sijawahi kushuhudia ubatizo wa Roho Mtakatifu, Ndugu Branham." Hilo ndilo ninalozungumzia. Hiyo ndiyo njia pekee mnaweza kuwa warithi wa ahadi, ni kupitia—ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unajua hilo. Huko ni kuzaliwa kwako. Huo ni mchanga wako mtakatifu. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki huko nyuma, mwanangu. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki huko nyuma. Hiyo ni sawa. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ewe kijana.

> Bwana, nijalie nitazame ng'ambo ya pazia la wakati.
>
> Acha niangalie ng'ambo ya pazia la huzuni na hofu,
> Acha nisikie kengele tamu ya bandari ikilia;
> Ingeangaza njia yangu na kuondoa hofu zote;
> Bwana, nijalie nitazame ng'ambo ya pazia la wakati.

114 Ikiwa umesimama mahali hapo, ambapo hujui mahali ulipo! Mikono kumi au kumi na tano imeinuliwa. Ninahisi kuwa kuna zaidi. Katika asubuhi hii ya Pasaka, kwa nini usiinue mkono wako na kusema, "Bwana, mimi hapa. Na kidimbwi hicho kitakapofunguliwa saa tano, nitakuwa moja kwa moja kwenye maji hayo, pia. Ninaenda kubatizwa, ili niweze kufufuliwa katika upya wa Maisha, kutembea pamoja nawe, Bwana. Ninataka kutazama ng'ambo ya pazia la wakati. Ninataka kuwa na tukio sasa hivi, asubuhi hii ya Pasaka, ambalo ninaweza kusema, wakati wowote katika maisha, 'Naam, nilikuwa nimeketi katika maskani ndogo ya zamani, asubuhi moja nzuri ya Pasaka. Mungu aliinua pazia. Nilitazama nyuma. Niliona kanisa langu halina maana sana. Niliona hakuna kitu duniani ambacho kilikuwa na maana sana kwangu tena. Hapo niliuza kila kitu nilichokuwa nacho. Nikanunua Lulu ya bei kubwa. Nikamkubali Yesu kama Mwokozi wangu.' Sasa ninainua mkono wangu, Bwana Mungu. Unirehemu. Mungu, nataka kutazama nyuma ya pazia la wakati." Je, kunaweza kuwa na mwingine kabla ya kufunga sasa hivi?

115 Mungu mpendwa, huu ni wakati adhimu. Tunafurahia baraka. Tumelifurahia Neno. Tumefurahia, zaidi ya tunavyoweza kueleza, Uwepo wa Roho Mtakatifu, Yule aliyetupa hakikisho hili kuu, kwamba tumepita, na tumepita kutoka—kutoka mautini kuingia Uzimani. Na kuna wale waliopo sasa, Bwana, wengi wao, wameinua mikono yao. Huu ni wakati adhimu.

116 Labda wanaweza kuwa wamefunzwa katika shule fulani ya kidini. Huenda wamewasha mishumaa. Huenda wamekariri

sala, juu ya shanga. Huenda wamejiunga na madhehebu fulani; wakazamishwa kwa njia fulani, kumwagiwa maji juu ya vichwa vyao, au kunyunyiziwa. Huenda wamekariri Kanuni ya Imani ya Mitume na kupitia utaratibu wa kitamaduni. Lakini hawajawahi kufika kwenye mchanga huo mtakatifu, hawajawahi kufika mahali hapo kama Ayubu alivyofanya, kama Musa, kama Ibrahimu, kama watoto Wako wote walivyofanya. Hawajafika mahali hapo kama wale wanafunzi waliokwenda kaburini, asubuhi ile, na kumkuta ameondoka.

117 Jalia, Bwana, sasa hivi, wale walioinua mikono yao, kwamba Roho Mtakatifu mkuu atakuja mioyoni mwao na kufanya kazi hii kuu ambayo tunaombea sasa. Utusikie, Bwana. Wao ni Wako. Wao ni matunda ya Ujumbe. Ninaomba ya kwamba utawabariki, kiajabu. Wape ubatizo wa Roho Mtakatifu, leo.

118 Na hatujui, huenda kamwe tusione Pasaka nyingine. Bila shaka kuna wengine hapa ndani ambao hawataona; si Pasaka kama hii, Pasaka kama ukumbusho. Lakini, Bwana, jalia waione hiyo Pasaka halisi, ile, Bwana, ambapo miili yao itaumbika katika umbo la kijana mwanamume au mwanamke, tena, watoke kaburini, ili kuishi milele.

119 Wabariki, Bwana. Wao ni Wako. Wewe ndiwe uliyewavuta. Kwa maana imeandikwa, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Sasa hao ni Wako, kama Wewe ndiye uliyewavuta. Ikiwa Wewe uko karibu nao vya kutosha, kuinua mikono yao juu hewani, Wewe uko karibu vya kutosha kufanya kazi iliyobaki. Wao ni Wako, Baba. Jalia kwamba huu uwe wakati wa amani kwao.

120 Asante kwa hawa wote ambao wamefanya uamuzi wao zamani, na kupitia maisha mapya, wakasimama kwenye mchanga mtakatifu. Tuko hapa kufurahi asubuhi ya leo pamoja nao, katika matumaini ya Kuja kwa Bwana Yesu, wakati sisi pia tuta—tutashirikiana Naye, katika ufufuo Wake, kama tulivyoshiriki katika mateso Yake. Tujalie, Bwana. Roho Wake na atutawale na kutuongoza, tunapoendelea na safari.

121 Tupe ibada kuu, sasa, saa tatu na nusu, Bwana. Na mara moja uwaponye wagonjwa na wanaoteseka.

122 Jalia wale ambao bado hawajazamishwa, waje kaburini asubuhi ya leo, waende chini, na kufufuka tena katika kaburi la maji hapa, Bwana, limeagizwa na Bwana wetu. Baada ya kufufuka Kwake alitokea na kusema, "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Aaminiye na kubatizwa ataokoka." Tujalie, Bwana, na itakuwa hivyo.

123 Utupe usiku mwema, usiku wa leo. Fanya, Baba, utupe siku kuu. Na tufurahie Uwepo wa Mungu kwa muda mrefu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

124 Kitu tu kuhusu wimbo huo wa zamani, unanifanyia jambo fulani tu! Wakati giza limeondoka, nini kilitokea? Nuru. Hebu tuimbe sasa, kwa utukufu wa Mungu. Kila mtu, pamoja sasa.

> Loo, tutatembea katika Nuru, Nuru nzuri,
> Inakuja ambapo umande wa rehema unang'aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

125 Alipokuja asubuhi ya Pasaka, alilivunja giza lote; alikimbia tu. Sasa Yeye anasimama kama Nuru. "Mimi ndimi ufufuo na Nuru, ufufuo na Uzima, ufufuo na maisha ya baadaye." Yote katika yote yako ndani Yake.

126 Hivi hamumpendi? Ni wangapi wanampenda? Inueni mikono yenu, juu sana. Hiyo ni nzuri.

127 Peana mikono sasa na mtu fulani anayeketi karibu nawe, tunapoimba tena.

> Tuta . . .

Kulia, kushoto, nyuma, mbele.

> . . . Nuru nzuri.
> Yesu . . .

128 Ibada zitafuata, sasa, saa tatu na nusu, na halafu kutakuwa na ibada ya mahubiri, maombi kwa ajili ya wagonjwa. Ibada ya ubatizo itaanza saa tano. Ninyi nyote mnaotaka kubatizwa, kwa kuzamishwa; kidimbwi kimejaa. Nitaleta nguo zangu. Tutarudi baada ya muda mfupi.

129 Ndipo, usiku wa leo, kuna ibada nyingine usiku wa leo, inakuja, mstari wa uponyaji, Ujumbe, na mstari wa uponyaji. Nasi tutaona, kile, aha, usiku wa leo ni usiku wa ushirika kwenye maskani, tena. Tutaona; tuna ratiba yenye shughuli nyingi sana, kwa hivyo itatubidi tufanye haraka sasa. Nendeni kwenye maeneo yenu mliyoandaliwa, mpate kiamshakinywa, na mrudi, mkishangilia.

130 Tunaposimama sasa na kuimba, "Anaishi, anaishi, Kristo Yesu anaishi leo." Vema, Ndugu Neville, tafadhali njoo huku.

> Anaishi, anaishi, Kristo Yesu anaishi leo!
> Anatembea nami na kuzungumza nami katika
> njia nyembamba ya maisha.
> Anaishi, anaishi, kuleta wokovu!
> Unaniuliza ninajuaje anaishi? Anaishi ndani
> ya moyo wangu.

131 Sasa, kila mtu, kwa sauti, "Haleluya!" "Haleluya!"

> Anaishi, anaishi, Kristo Yesu anaishi leo!
> Anatembea nami na kuzungumza nami katika
> njia nyembamba ya maisha.
> Anaishi, anaishi, kuleta wokovu!

Unaniuliza ninajuaje anaishi? Anaishi ndani
ya moyo wangu.

132 Hebu tuuimbe tena. Tukifika hapo, “Anaishi, anaishi,” hebu tumwinulie mikono yetu, namna *hiyo*. “Anaishi, anaishi. Unaniuliza ninajuaje anaishi? Anaishi ndani ya moyo wangu.” Kila mtu sasa.

Anaishi, anaishi, Kristo Yesu anaishi leo!
Anatembea nami, anazungumza nami katika
njia nyembamba ya maisha. (. . .?. . .)
Unaniuliza ninajuaje anaishi? (Vema, sasa.)
Anaishi ndani ya moyo wangu.

133 Yeye si ni wa ajabu? Wakati huu mtakatifu, mtukufu sasa, ambapo tumeachiliwa, kwenda nyumbani kwetu kwa kifungua kinywa chetu. Turudi, tukifurahi.

134 Nitauliza, tunapoinamisha vichwa vyetu, kama mpendwa wetu Ndugu Foulst hapa, kutoka Kanada, ikiwa atatuhusu tuondoke kwa maombi. Ndugu Foulst, tafadhali.

Najua Mkombozi Wangu Yu Hai SWA58-0406s
(I Know My Redeemer Liveth)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili ya Pasaka kwenye mapambazuko asubuhi, tarehe 6 Aprili, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org